JAMHURI KENYA
SERIKALI YA KAUNTI YA NYERI
S.L.P 1112 – 10100, NYERI, Barua-pepe: lands@nyeri.go.ke
IDARA YA ARDHI, MIPANGO YA USTAWI NA USTAWISHAJI WA MIJI

# ILANI YA DHAMIRA YA KUANDAA MIPANGO YA KIENEO YA USTAWISHAJI NA MATUMIZI YA ARDHI

**Jina la Mipango ya Maendeleo** - Mipango ya Kieneo ya Ustawishaji na Matumizi ya Ardhi ya vijiji vya kikoloni vya **Gathaithi, Mathaithi, Ndumanu, Mununga-ini, Muthathini, Ragati na Tambaya.**

Kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha (47) cha Sheria ya Mipango ya Ustawishaji na Matumizi ya Ardhi, 2019, ILANI inatolewa kwamba Serikali ya Kaunti ya Nyeri inanuia kuanza utayarishaji wa Mipango iliyotajwa hapo juu tarehe 27, 2024.

**Madhumuni ya mipango hiyo ni:**
Kuelekeza ustawishaji wa vijiji hivi kwa njia jumuishi na kwa utaratibu bora ili kufaulisha maendeleo endelevu na kuweka msingi wa utoaji wa miundomsingi, makazi na milki za umma.

**Malengo ya Mipango hii ni:**

i) Kuimarisha matumizi bora ya ardhi kama rasilimali adimu
ii) Kuimarisha taratibu pendelevu na madhubuti za matumizi ya ardhi
iii) Kubuni msingi wa ustawishaji miundomsingi, makazi na milki za umma.

Maoni kuhusu mipango hiyo iliyopendekezwa yanaweza kutumwa kwa:

**Waziri wa Kaunti (CECM)**
**Ardhi, Mipango ya Ustawi & Ustawishaji wa Miji**
**Serikali ya Kaunti ya Nyeri**
**S.L.P 1112-10100, Nyeri.**

**Ndani ya siku 14 kuanzia tarehe ya kuchapishwa kwa tangazo hili.**

**Tarehe: 13 Mei 2024**

**Mhesh. Ndirangu Gachunia**
Waziri wa Kaunti